**9 JUNI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Arobaini na Nne – Tarehe 9 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 567

**Kupeleka fedha za maendeleo kwenye Halmashauri**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali haipeleki fedha za maendeleo kwa wakati katika Halmashauri nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa niaba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikipeleka fedha kwa wakati, mfano hadi kufikia mwezi Mei, 2023 kiasi cha shilingi trilioni 1.08 sawa na 116% zilipelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kote.

Mheshimiwa Spika, miradi inayotekelezwa na wakandarasi fedha hutolewa kulingana na hati ya madai ya kazi kulingana na utekelezaji wa majukumu hayo. Aidha, kwa miradi linayofanywa na *force account,* fedha hutolewa kwa kuzingatia utayari wa Halmashauri wa kuanza utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa taratibu hizi unatolewa kulingana kwa mujibu wa kanuni na mwongozo wa utoaji fedha katika utekelezaji wa bajeti za Serikali ya mwaka 2021 iliyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza nishukuru kwa majibu, lakini Serikali imesema itasimamia mikoa ili iweze kusimamia Halmashauri zisizo na utayari wa kuanza kutekeleza miradi.

Mheshimiwa Spika, lakini mikoa yenyewe imekuwa na chagamoto ya kuwa na fedha ambazo zinafanya ufatiliaji, tumekuwa tukiona tukienda ndio tunakwenda nao.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha kifedha Sekretarieti za Mikoa ili zitekeleze wajibu wao ipasavyo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; fedha hizi hutolewa chini ya masharti ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982; zipo Halmashauri zinapata fedha zaidi ya walichoomba na ziko Halmashauri zinapata pungufu ya walichoomba na zipo zinazocheleweshewa kabisa kupata kuanzia mwezi wa tano hadi wa sita, na Halmashauri zinazopata zaidi zinafanya ubadhirifu wa kutumia fedha zaidi nje ya matumizi ambayo walipanga na nyingine zinazopata kidogo hazitekelezi mikakati yao kikamilifu. *(Makofi)*

Je, Serikali ina mkakati gani na kauli gani tunaipata kutoka kwa Serikali kuhusu suala hili? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Grace Victor Tendega kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na fedha zinazotakiwa kupelekwa katika mikoa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, fedha zote zinazopelekwa katika maeneo yote kwa mujibu wa kanuni ambayo yeye mwenyewe amei–*cite* inayotoa miongozo ya fedha, inataka wahusika waombe fedha TAMISEMI ili wapelekewe na kama yako maeneo ambayo yametokea mapungufu hayo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutafatilia na tungeomba taarifa hizo utupe za kina ili tuweze kuzifatilia.

Pili juu ya upendeleo; nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali haifanyi upemndeleo na kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, miradi inayotekelezwa ndio ambayo inaielekeza Serikali ifanyeje, katika *force account* kinachofanyika ni kwamba Halmashauri husika inapokuwa tayari kutekeleza mradi inatoa taarifa kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, na fedha zinapelekwa na katika ilani ambayo inasimamiwa na wakandarasi Serikali inachofanya ni kwamba baada ya mkandarasi ku-*raise certificate* basi Serikali inapeleka pesa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nikuhakikishie na Bunge lako kwamba Serikali iko makini inaendelea kufanya kazi vizuri na kama yako mapungufu katika maeneo ambayo wewe Mheshimiwa Mbunge umewahi kupita, basi utupe taarifa tuweze kufatilia na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 568

**Mkakati wa kufanya mageuzi ya kilimo nchini**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kufanya mageuzi ya kilimo nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali wa kuleta mageuzi ya kilimo. Mikakati hiyo inatekelezwa kwa lengo la kubadili kilimo kutoka kilimo cha kujikimu kuwa kilimo biashara, chenye tija, himilivu kinachoratibiwa na kusimamiwa na Serikali na kushirikisha sekta binafsi ili kuwa na mifumo endelevu ya chakula na kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia misingi hiyo ya kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo, Serikali kupitia bajeti ya mwaka 2023/2024 inatekeleza vipaumbele mikakati yenye lengo la kuongeza tija na uzalishaji; kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo; kuimarisha usalama wa chakula na lishe; kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya nje ya nchi na kuimarisha maendeleo ya ushirika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pamoja na majibu haya mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza je, Serikali sasa ina mpango gani mahususi wa kuwapatia wakulima nchini zana za kisasa za kilimo hususani matrekta ambapo sasa hivi tunaona wananchi wetu wanatumia jembe la mkono katika maeneo mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali ina mpango gani mahususi wa kufanya kilimo cha umwagiliaji kuwa ni ajenda ya kitaifa ambapo wananchi wetu sasa waweze kulima mara mbili kwa mwaka kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua. Tuna maeneo mengi yenye maji kama Singida Kaskazini, lakini bado

hayajatumiaka ipasavyo. Tunaomba mkakati mahsusi wa Serikali kuhusu ku–*mechanize* kilimo chetu.

**SPIKA:** Umeshauliza swali Mheshimiwa.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Nimeshauliza.

**SPIKA:** Ndiyo. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nikianza na swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge kuhusu zana za kilimo kama alivyosema tunaendela kufanya mageuzi katika matumizi ya zana za kilimo za kisasa ili wakulima wetu waweze kuzalisha kwa tija na hivi sasa tunashirikiana na *CARMTEC* na Shirika la *TEMDO* katika kuja na teknolojia mbalimbali na zana mbalimbli za kusaidia katika uzalishaji katika sekta hii ya kilimo. Lakini kubwa kuliko yote ni kwamba tunakwenda kuanzisha *mechanization hub* katika ikolojia mbalimbali za nchi yetu ya Tanzania kikanda ili wakulima wetu pia waweze kutumia fursa hiyo ya kuweza kutumia mitambo hiyo ya kukodisha badala ya mkulima kwenda kukopa trekta huko ana ekari mbili na kuingia gharama kubwa, tunaweka vituo hivi kwa ajili ya ukodishaji wa zana za kilimo za kisasa.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu mipango mahususi katika eneo la umwagiliaji, kama nilivyokuwa nikisema hapa ndani ni dhamira ya Serikali kuhakikisha ya kwamba tunatekeleza kwa dhati kabisa eneo hili la umwagiliaji kwa kuweka mipango madhubuti na mkakati mkubwa hivi sasa ni kuhakikisha *scheme* zetu zote za umwagiliaji nchini zinafanya kazi, lakini hatua kubwa na ya kwanza ni kuhakikisha kwanza tunaweka vyanzo vya uhakika vya maji ili *scheme* hizo ziweze kufanya kazi na wananchi waweze kuhudumia mashamba yao zaidi ya mara moja ndani ya mwaka mmoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe maswali mafupi, kipindi cha maswali siyo kipindi cha kuchangia. Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi, pamoja na mkakati uliosema wa kugeuza kilimo kama cha biashara.

Je, kuna mkakati gani kwenye eneo la Yaeda Chini na Eshkesh ambayo ni kame unavyojua kuyageuza maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, samahani sijamsikia.

**SPIKA:** Mheshimiwa uliza swali, Serikali inaelewa yaani usianze na taarifa za mwanzo, unaona Waziri hajasikia swali lako. Muulize swali.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Kata ya Yaeda Chini na Eshkesh ina ukame, je, katika mpango wako ni namna gani ya kusaidia kata zile kwa ajili ya kilimo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, tunakwenda kuanzisha ukanda wa kilimo wa kikanda nchi nzima ili kuweza kuyafikia maeneo yote kutokana na ikolojia, kwa hiyo, na maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja kupitia utaratibu huu tutaweza kuyafikia na kuwasaidia wakulima wetu kulima kwa tija.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

Mheshimiwa Felix Kavejuru swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa mbolea na pembejeo za kilimo zitafika mapema kabla ya mvua za mwanzo hazijanyesha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, Serikali imekwisha kutamka narudia tena huku kwamba tutahakikisha wakulima wetu hawapati changamoto zilizojitokeza katika msimu uliopita, mbolea ya kupandia na kukuzia itaanza kuingia mwezi wa saba mapema kabisa ili wakulima waweze kununua na uhifadhi kwa ajili ya msimu unaokuja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, sasa aulize swali lake.

Na. 569

**Umeme kufika kwenye vitongoji vyote nchini**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha umeme unafika kwenye vitongoji vyote nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* imekamilisha uhakiki wa vitongoji 36,101 visivyokuwa na huduma ya umeme na kuandaa mradi kabambe wa kusambaza umeme katika vitongoji vyote uliopewa jina *Hamlet Electrification Project (HEP)* vikiwemo vijiji 262 vya Wilaya ya Rorya. Mradi huu utagharimu takribani shilingi 6,700,000,000,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha mipango ya upatikanaji wa fedha hiyo na mradi huu unatarajiwa kutekelezwa ndani ya miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2024. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Jimbo la Rorya litapatiwa fedha kutoka *REA* ya kufikisha umeme katika vitongoji 15 vya kuanzia, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nataka nijue ni lini sasa *REA Phase Three Round Two* ya kusambaza kilometa mbili za ziada kwenye Wilaya ya Rorya utaanza kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili. Kampuni tanzu ya *ETDCo* imepewa kazi zaidi ya miaka mitatu sasa kusambaza umeme wilaya ya Rorya, lakini mpaka sasa hawajaanza kufanya kazi.

Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kumfuta mkandarasi huyu ili itangaze upya waombe wakandarasi wengine kwa ajili ya kusambaza umeme Wilaya ya Rorya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, leo tunatarajia wenzetu wa *REA* watasaini baadhi ya mikataba ya *extension* ya kilomita mbili kwa kila kitongoji na tunaamini kufikia mwishoni mwa mwezi huu wakandarasi hao watafika *site* ili kuanza kufanya kazi hizo za kuongeza hizo kilometa mbili kwenye maeneo ambayo mikataba ya vijiji imekamilika na pengine inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la pili, naomba baada ya hapa nikae na Mheshimiwa Chege ili tuone tatizo liko wapi kwa sababu tunafahamu miradi mingi inaendelea kwa hatua mbalimbali katika maeneo yetu, *specifically* nitakaa ili tubaini changamoto aliyoiona iko wapi na tuweze kueleweshana na kuchukua hatua stahiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafai hii.

Je, Serikali itamaliza lini ujenzi wa kituo cha kupozea umeme kinachojengwa katika Kijiji cha Uhuru, wilayani Urambo ili kumaliza tatizo la umeme tulilonalo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, mradi wa kujenga kituo cha kupoza umeme cha Uhuru kilichoko Urambo ni mojawapo ya miradi yetu 14 ya kujenga vituo vya kupoza umeme kwenye Wilaya inayotekelezwa chini ya mradi wetu wa Gridi Imara. Mradi huo tayari umeshaanza na tunatarajia ndani ya miezi kama 12 kuanzia sasa mradi huo pia utakuwa umekamilika katika eneo la Uhuru ili kuhakikisha kwamba umeme unaotoka Tabora kwenda Uhuru kwenda Nguruka basi unawafikia wahitaji kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge wa Ngorongoro sasa ulize swali lake.

Na. 570

**Hitaji la mawasiliano – Ngorongoro**

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka mawasiliano katika Kata za Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Mhandisi Kundo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* ilifanya tathmini na kubaini changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro na imekwisha wapata watoa huduma watakaofikisha huduma za mawasiliano katika Kata za Alailelai, Alaitolei, Engaresero, Mundarara, Ngoile, Olbalbal na Ololosokwan. Aidha, Serikali itayaingiza maeneo mengine yaliyobaki yenye changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, moja ya kata ulizotaja, kata ya Mundarara haipo Wilaya ya Ngorongoro, ipo wilaya ya Longido. Je, mpo tayari kubadilisha mnara ambao ulikuwa uende Kata ya Mundarara Kwenda moja kati ya wilaya za Ngorongoro?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni lini Serikali, itapeleka mawasiliano katika vijiji vya Kinaga, Loswashi, Nan pamoja na Osorosapia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Shangai kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, napokea mabadiliko haya lakini itabidi tukutane ili tuweze kulifanyia uchunguzi wa kina ili tuweze kuona kwamba tunafanya nini. Tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba tatizo hili linatatuliwa.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kwamba katika kata ambazo amezitaja Serikali iko katika tathmini. Tathmini mpaka sasa tumeshafikisha vijiji 2,224 na tunaamini kwamba tathmini ikishakamilika na Mheshimiwa Rais tayari ameshapata fedha kwa ajili ya kujenga minara mingine 600. Kwa hiyo, tunaamini katika hizo kata zitaingizwa katika ya utekelezaji wa minara ambayo itakuja kwa awamu inayokuja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itapeleka na kujenga minara ya simu katika kata zenye shida kubwa ya mawasiliano ya simu yaani Serengeti ikiwemo Busawe, Issenye, Kenyamonta, Manchira, Mbalibalim Nagusi, Natta, Nyamatare, Nyambureti, Nyamoko na Uwanja wa Ndege?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amsabi Mrimi, Mbunge wa Serengeti kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kbisa Mheshimiwa Mbunge ameshaleta changamoto ya maeneo ambayo yana changamoto ya mawasiliano, lakini katika kata ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge isipokuwa Kata ya Uwanja wa Ndege na ndio ambayo

hatutaiingiza katika mpango huo wa utekelezaji. Zingine zote tutaziingiza katika utekelezaji, ahsante sana.

**SPIKA:** Sasa hiyo ambayo hamuiingizi ni kwamba mnao mpango wa baadaye ama? Maana wananchi sasa wakisikia kwamba hii ndio haiingizwi kwenye mpango?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameshaleta changamoto hizo na tayari tulizipokea, ametaja hizo Kata nazikumbuka isipokuwa ya Uwanja wa Ndege ambayo hakuileta, sasa hiyo itabidi isubiri mpango wa awamu ijayo ili iweze kuingizwa, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ningependa kujua ni lini Serikali itajenga minara katika maeneo ya Mkoa wa Kagera ambayo ni pori la Kimisi lakini pia Pori la Biharamulo, ni mapori hatarishi na wakati mwingine mtu akipata ajali au..

**SPIKA:** Unatoa mchango Mheshimiwa?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, sawa, naomba kujua ni ni lini maeneo haya hatarishi yatawekewa mawasiliano kwa ajili ya kuokoa maisha ya watu.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANONA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya mikoa ambayo imepata minara mingi sana katika minara 758 ni Mkoa wa Kagera, lakini kwa sababu

Mheshimiwa Mbunge ameonyesha changamoto iliyopo katika maeneo ya mabonde, mapori pamoja na maeneo mengine, tutatuma timu yetu ya wataalam wetu, wataenda kujiridhisha na ukubwa wa changamoto hizo ili tujue hatua gani tutachukua kutatua changamoto hiyo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH. G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, maeneo kama Mwamayunga, Isongwa, Ipembe, lini nayo yatapata minara ya simu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANONA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kakunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ambazo amezitaja tayari tumeziweka kwenye tathmini katika vijiji 2224 na tayari Mheshimiwa Rais ameshapata fedha kwa ajili ya minara 600 na baada ya 600, kuna minara mingine 1,000 inakuja, kwa hiyo tukitoka hapa leo tukae Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuyapanga vizuri kwa ajili ya wananchi wa Jimbo lake ili waweze kupata huduma ya mawasiliano, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA ALLY MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hali hiyo inafanana pia katika Kata za Lipumbulu, Sinano, Lupaso na Mchauru katika Jimbo la Lulindi, ni lini zitapatiwa minara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANONA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungahela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mheshimiwa Mchungahela pamoja na Kata ambazo amezitaja, zipo katika minara 758 ambayo tayari utekelezaji wake umeshaanza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Florence Geoge Samizi, Mbunge wa Muhambwe, sasa aulize swali lake.

Na. 571

**Ukarabati wa Kituo cha Polisi pamoja na nyumba za askari – Kibondo**

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati kwenye Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kibondo pamoja na nyumba za Askari Polisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu, Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kibondo pamoja na nyumba za makazi ya Maofisa na Askari ni chakavu.

Tathmini ya uchakavu kwa ajili ya kufanya ukarabati imefanyika na kiasi cha Sh.28,914,250/= kinahitajika kwa ajili ya kukarabati Kituo cha Polisi na Sh.109,288,000/= zinahitajika kwa ajili ya ukarabati wa nyumba nane za makazi ya Maofisa na Askari Polisi. Kulingana na hali ya upatikanaji wa fedha, Serikali imepanga kutekeleza ukarabati huo katika mwaka wa fedha 2024/2025, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza kabisa naishukuru Serikali kwa majibu mazuri ambayo yameonesha matumaini kwa kuwa wameshafanya tathmini, lakini, je, Serikali haioni kwamba iko sababu ya kuharakisha ukarabati wa nyumba hizi ili kuboresha ufanisi wa askari angalau kwa kuanza na pesa kidogo mwaka huu, *then* mwaka kesho tumalizie? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, haja ya kufanya haraka ya kuharakisha upatikanaji wa hizi huduma ni jambo la msingi na sisi kama Wizara tutahakikisha kwamba tunakwenda kutafuta fedha kokote ziliko ilimradi tuhakikishe kwamba Vituo vya Polisi nchini kote ikiwemo Jimbo la Mheshimiwa Mbunge la Muhambwe vituo hivi vifike.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu ya azma njema ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba kwanza wananchi wote wanapata huduma za ulinzi na usalama, lakini pia kuhakikisha kwamba tunaboresha mazingira yawe mazuri zaidi kwa upande wa vyombo hasa Jeshi la Polisi ikiwemo magari na Vituo vya Polisi na nyumba za makazi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je ni lini Serikali sasa itamaliza nyumba za askari eneo la *Barracks Kilwa Road* ndani ya Jimbo la Temeke?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba Vituo vyote vya Polisi ikiwa vya Wilaya ikiwa vya Mikoa itahakikisha kwamba vinakamilika, lengo na madhumuni wananchi wajue sasa wapi wanakwenda kupeleka changamoto zao, kwa sababu tumegundua bado kuna baaadhi ya maeneo yakiwemo wilaya na maeneo mengine bado hayajapata Vituo vya Polisi. Kwa hiyo nimwambie tu Mheshimiwa kwamba tutahakikisha kwamba Kituo cha Polisi kinakuja na fedha zitakapopatikana, tutahakikisha kwamba tunampa kipaumbele kwa ajili ya kupata hicho Kituo cha Polisi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Uvinza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inatambua umuhimu wa uwepo wa Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Uvinza. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi. Kokote tutazitafuta fedha zilipo ili tuhakikishe kwamba tunapeleka Kituo cha Polisi katika Jimbo lake ili mradi wananchi

waweze kupata huduma za ulinzi na usalama na mambo mengine ya kipolisi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Je ni lini Serikali itaweka bayana mpango mzima wa ukarabati au ujenzi wa Vituo vya Polisi pamoja na nyumba za kuishi kwa nchi nzima ili kuepuka kudaiwa huduma hii kila kukicha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshaanza kufanya tathmini ya kuona namna ambavyo tunaweza tukauandaa huo mpango. Kwa hiyo nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi kadiri iwezekanavyo tuone namna ambavyo tunauhangaikia huo na kuweza kuanza kuufanyia kazi kama ambavyo Mheshimiwa ametaka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika Kijiji cha Mkundoo na Mkusinde kumekuwepo na matukio kadhaa yameripotiwa ya uhalifu. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi eneo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumekuwa tukiripotiwa baadhi ya matukio ambayo mengi yao yamekuwa yakisababishwa na wananchi wenyewe kwa wenyewe, lakini nimwambie tu kwamba Serikali haijalala kwa maana kwamba ipo makini kuhakikisha

kwamba tunapambana dhidi ya vitendo vyote vya uhalifu ikiwemo na kuhakikisha kwamba tunatafuta magari kwa ajili ya kufanya doria na ukaguzi wa mara kwa mara ikiwemo na kujenga Vituo vya Polisi kwa ajili ya wananchi ili kuweza kwenda kupeleka changamoto zao na kuweza kutatuliwa kwa haraka, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka Mbunge wa Liwale, sasa aulize swali lake.

Na. 572

**Hitaji la Kituo cha Polisi Liwale**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za ujenzi wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Liwale?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale imetoa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 10,000 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi pamoja na nyumba za makazi ya askari. Tathmini ya makadirio na michoro kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi, daraja B umeshafanyika na kiasi cha Sh.768,024,734/= kinahitajika. Fedha hizo zitatolewa kwenye Mfuko wa Tuzo na Tozo katika mwaka wa fedha 2023/2024, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa mara ya kwanza swali langu hili limepata majibu mazuri ya Serikali, imenitia tumaini, lakini bado ina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa sababu ya kituo hiki kuitwa kituo cha karibu cha usaidizi Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja Liwale alituahidi kutujengea kituo kwenye Tarafa ya Kibutuka na Kata ya Lilombe. Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa sababu jiografia ya Liwale kuwa ngumu hali ya usafiri ni mbaya sana, sasa je, Serikali iko tayari kutupatia gari kwa ajili ya maaskari wa kituo hiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, najibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kuchauka kwamba ahadi zote zilizoahidiwa na viongozi wa Serikali zitatekelezwa. Sasa hivi tupo kwenye kufanya tathmini kuona wapi paliahidiwa ili tuanze sasa utekelezaji wa ahadi hizo. Kwa hiyo hicho ambacho kimeahidiwa Mheshimiwa awe na amani kitatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kingine nimwambie ni kweli Serikali inafahamu umuhimu wa uwepo wa magari katika meneo mengi ambayo watu wanaishi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, kwanza tunafanya *operation* za mara kwa mara, lakini kufanya doria za mara kwa mara na kuhakikisha kwamba tunapambana na matukio ya kihalifu. Nimwambie tu Mheshimiwa kwamba katika gari ambazo zitafika tutahakikisha kwamba katika Jimbo la Liwale gari itakwenda ili iweze kusaidia wananchi kwa ajili ya kuweka hali ya amani na utulivu katika eneo hilo, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa. Serikali imepeleka Polisi Kata kwenye kila Kata katika nchi hii kwenye *rank ya inspector,* lakini mapolisi hawa hawana ofisi wala makazi kwenye haya maeneo. Je, Serikali ina mpango gani kuwapelekea vijana wetu hawa kuwajengea Ofisi na nyumba za kuishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua kwamba kuna baadhi ya Ofisi zimekuwa zimechakaa kwa sababu ni za muda mrefu, lakini vilevile tunatambua kwamba kuna maeneo mengine hata hizo Ofisi zinakuwa changamoto, lakini nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi, kama ambavyo tumejibu katika majibu yetu ya msingi, tutajitahidi kuhakikisha kwamba kila mahali wanapata Vituo vya Polisi, lakini kila mahali wanapata nyumba za makazi kwa ajili ya Askari Polisi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itawajengea askari polisi wa Wilaya ya Kilolo kwa sababu hawajawahi kujengewa nyumba, wanaishi kwenye nyumba za kupanga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeanza kutoa maibu yangu kwamba, tutahakikisha katika bajeti ambayo tumeeleza hapa katika jibu letu la msingi, tutahakikisha kwamba tunaanza ama tunaendeleza kujenga nyumba za makazi, kwa sababu kama tulivyosema mwanzo hiyo changamoto tunaifahamu na tunajua

kwamba askari wetu wengi wanaishi kwenye nyumba nyingi zimechakaa, lakini tutahakikisha kwamba tunawajengea nyumba na makazi ya kisasa ili waweze kukaa kwenye makazi mazuri na kuweza kutoa huduma vizuri kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu Mbunge wa Kibamba, sasa aulize swali lake.

Na. 573

**Tatizo la maji - Jimbo la Kibamba**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

Je, ni lini Wananchi wa Mpiji – Magohe, Kibesa, Msumi, Makabe, Msingwa, Ukombozi na Goba watapata majisafi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ukamilishaji wa Miradi ya Maji ya Changanyikeni - Bagamoyo, ujenzi wa matenki ya maji katika maeneo ya Mshikamano, Tegeta A, Malolo na mradi wa usambazaji maji kusini mwa Dar es Salaam ambapo kukamilika kwa miradi hii kutawezesha wakazi wa maeneo ya Mpiji-Magohe, Kibesa, Msumi, Mbezi, Makabe, Msakuzi, Msingwa, Ukombozi, King'azi,

Malamba Mawili, Msingwa, Kipesa Mapwepande, Mpakani na Goba kupata huduma ya majisafi, salama na ya kutosheleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, ni dhahiri nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa utekelezaji wa miradi hii iliyotajwa na Serikali, tunawashukuru sana Serikali. Pamoja na changamoto sasa iliyopo tayari miradi ya Tegeta A na Mshikamano tunayo mizuri usambazaji wa mabomba umekuwa ni changamoto sana kwa sababu ya yale maboza, magari yanayouza maji kwa wananchi…

**SPIKA:** Swali lako Mheshimiwa.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwa sababu tayari wanatakiwa wasambaze watoe kauli hapa ya kusitisha uuzaji wa maji kwa magari. Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa kuna mradi huo wa usambazaji maji…

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, hebu ngoja kwanza, Naibu Waziri kwa sasa hivi hasikilizi mchango, anataka swali ili akujibu kwa sababu hiki ni kipindi cha maswali na majibu. Muulize swali Naibu Waziri akujibu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza Serikali mpo tayari kutoa kauli ya usitishaji wa uuzaji wa maji kwa magari Jimbo la Kibamba kwa sababu mlishatekekeleza miradi miwili kule?

**SPIKA:** Haya ahsante sana, la pili.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu King'azi hakuna maji kabisa wanatumia maji ya chumvi, ni lini mradi wa usambazaji Dar es Salaam Kusini utaanza?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtemvu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uuzaji wa maji kwenye magari hili suala tulishalipigia marufuku kwa maeneo mengi na hususani eneo la Kibamba, lakini tutaendelea kuhakikisha kwanza tunahakikisha miradi ile imekamilika na uhakika wa maji ya uhakika wa kila siku kwa wananchi, suala hili naamini litatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, suala la Dar es Salaam kusini maeneo ya King'azi usambazaji wa mabomba, tunatarajia mapema mwaka wa fedha ujao kuanzia mwezi Julai au Agosti, suala la usambazaji wa mabomba katika maeneo haya yote aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge tunakuja kuyafanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Jiji la Dodoma limekuwa lina matatizo sana ya upatikanaji wa maji na hivyo kuwa kero kubwa sana kwa wananchi. Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kupunguza tatizo hili ili kusudi wananchi waweze kufaidika na maji safi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dodoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali kwa Jiji la Dodoma Waheshimiwa Wabunge naamini ni mashahidi tunaendelea kufanya kazi nyingi sana kuona tunakwenda kukomesha tatizo la maji katika Jiji la Dodoma kwa umuhimu wake kama Makao Makuu ya Nchi tuna miradi mingi mikubwa, ya kati na midogo, tunatarajia mwaka

ujao wa fedha miradi mingi itaanza kupeleka huduma ya maji maeneo yote ambayo yanapata changamoto.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi ya maji katika Kata ya Duru na Yasanda, Jimbo la Babati Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Babati Vijijini, Miradi ambayo ipo kwenye utekelezaji tunaendelea kupambana kuona inakamilika ndani ya wakati na maeneo ambayo usanifu umekamilika pia mwaka ujao wa fedha tutaendelea kuongeza nguvu katika maeneo yote ya Babati Vijijini ili kupata maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza, je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya maji katika Tarafa ya Ngerengere?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamisi Taletale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Ngerengere tayari tuna miradi ambayo ipo kwenye utekelezaji, lakini tuna mipango thabiti ya kuona kwamba eneo hili nalo linaenda kupata huduma ya maji safi

na salama mwaka ujao wa fedha Mheshimiwa Mbunge atashuhudia shughuli nyingi sana zikifanyika katika Tarafa hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Wizara ya Maji itaanza kujenga au kutekeleza Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya Wilaya ya Muleba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ziwa Victoria kwa Muleba Mheshimiwa Mbunge alikuja tukaongea na menejimenti, tulishakubaliana mwaka ujao wa fedha tunakwenda kukamilisha usanifu na kuanza kuona uwezekano wa kufanya mradi huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itapeleka Mradi wa Maji katika Kata ya Kalulu na Kata ya Jakika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata hizi alizozitaja mwaka ujao wa fedha tunatarajia kupeleka maji safi na salama kwa kupitia visima vilevile maeneo mengine tutatumia vyanzo vile vilivyo vya uhakika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi Mbunge wa Ukerewe, sasa aulize swali lake.

Na. 574

**Kumaliza kero ya maji – Ukerewe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali kumaliza kero ya upatikanaji wa maji safi na salama Wilayani Ukerewe?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ukerewe ina jumla ya vijiji 76, kati ya vijiji hivyo 37 vinapata huduma ya maji safi na salama. Aidha, katika mwaka 2022/2023, Serikali inatekeleza miradi katika vijiji vingine 26 na inatarajia kukamilisha miradi hii mwezi Julai, 2023.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali itajenga miradi ya maji kwenye vijiji 13 vilivyobaki ambapo ni Bugula, Kameya, Halwego, Chamuhunda, Mukunu, Bugorola, Kamasi, Busumba, Kaseni, Bukonyo, Busagami, Msozi na Kweru. Kukamilika kwa miradi hiyo kutaondoa kero ya maji Wilaya ya Ukerewe na wananchi wote watapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nitumie nafasi hii kwanza kutoa pongezi na shukurani kwa Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla kwa hatua mbalimbali zinazofanyika kuhakikisha Visiwa vya Ukerewe vinapata maji safi na salama. Swali

langu, Serikali sasa iko tayari kutoa maelekezo ili wakati wa usambazaji wa maji wataalam wazingatie mtawanyo kuhakikisha kwamba kila kitongoji kinafikishiwa mtandao huu wa maji? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Mkundi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napokea shukrani zako na wewe nakupongeza kwa sababu umekuwa mfuatiliaji na tumekwenda Ukerewe zaidi ya mara mbili mimi na wewe na kazi nzuri unaifanya.

Mheshimiwa Spika, suala la usambazaji maji kwa kila kitongoji, hiyo ni moja ya mipango ya Wizara. Nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo tumeweza kutatua changamoto ambayo ilikutesa kwa muda mrefu, suala la usambazaji maji pia tunakuja kulifanyia kazi na nitoe wito kwa Mameneja wote wa Wilaya ambao wananisikiliza waweze kuhakikisha wanafika katika vitongoji vyote na maji yanasambazwa kadri ya miradi ilivyosanifiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba swali la nyongeza.

**SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga kupeleka shilingi bilioni 195 ili kumaliza changamoto ya maji katika Mkoa wa Shinyanga. Nataka kujua Serikali imefikia wapi kutekeleza mpango huu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salome Makamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuleta shilingi bilioni 195 katika eneo la Shinyanga ni miradi ya kimkakati ambayo Wizara tunaendelea kutafuta fedha. Mara tutakapopata fedha tutaendelea kuzileta kwa awamu ili kuhakikisha mradi huu unatekelezeka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji katika Kata ya Bonyokwa Jimbo la Segerea. Je, ni lini changamoto hii itakwisha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge Viti Maalum kuwa maeneo ya Segerea, Bonyokwa tuna miradi ambayo iko mwishoni kabisa kukamilika, tunatarajia mapema mwaka wa fedha ujao maeneo haya yote yanakwenda kupata huduma ya maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, mradi wa maji Kiwira unaanza lini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu kabisa naomba kujibu swali hili kwa heshima kubwa.

Mheshimiwa Spika, mradi umeshaanza kutekelezwa kwa maana ya kwamba tayari maeneo kama ya *New Forest* na Mchangani Mkandarasi ameshaanza kujenga *camp* ili kuona kwamba anafanya *mobilization* lakini maeneo ya *Intake* na maeneo ya Sistila kule juu karibu ya *MUST* wanaendelea na *clearance* kwa ajili hiyo ya kujenga *camp* kuona kwamba kazi zitaanza mara moja lakini suala lililoko mezani kwa sasa hivi, tayari Wizara ya Fedha

imetoa *exchequer* ambayo imeingia kwenye Wizara ya Maji ukiisoma unaiona sasa hivi tunachosubiri tu ni fedha kuingia kwenye *account* na mamlaka kuweza kuingiziwa hiyo fedha mara moja Mkandarasi alipwe aendelee na mradi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hiyo hela zinachelewa wapi kwenu au Wizara ya Fedha?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri anakuja hapa kujibu sawa. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako. Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga Mbunge wa Mtwara Mjini, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 575

**Kuwasaidia wananchi waliojiunga na PRIDE kurudishiwa fedha zao – Mtwara Mjini**

**MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawasaidia Wananchi wa Mtwara Mjini waliojiunga na *PRIDE* kurejeshewa fedha zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya tathmini ya hali ya Kampuni ya *PRIDE* na kufuatiwa na ukaguzi maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kuhusu kutambua

mali na madeni ya kampuni hiyo. Kufuatia tathmini hiyo, Serikali inaendelea na taratibu za kisheria za kuifilisi *PRIDE*.

Mheshimiwa Spika, Madeni yatalipwa kwa kuzingatia sheria na taratibu za ufilisi na yanatarajiwa kukamilishwa ifikapo Julai 2023. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Mheshimiwa Waziri aliahidi kuja Mtwara kuzungumza na wadeni hao. Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kuja Mtwara kuja kuzungumza na hawa ambao wana wadai? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wananchi wa Jimbo la Mtwara wameahidiwa mara kwa mara juu ya majibu ya Mheshimiwa Waziri. Sasa ni lini sasa mtakuja kuwapa fedha zao hao wananchi wa Mtwara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hassan Mtenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi niko tayari kabisa kwenda kuwasikiliza na kukaa na wananchi wa Mtwara Mjini kuhusu madai yao mara tu baada ya Bunge kumalizika tutakaa na Mheshimiwa Mtenga tuende kukutana na wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba taratibu za ufilisi zinaendelea na kuanzia Julai mwaka wa fedha unaokuja tunaenda kuwalipa wananchi kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, kumekuwa na taarifa kwa wachuuzi wadogo wadogo maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Wilaya ya Nyang'hwale, kwa kupungukiwa na *silver* ama sarafu ndogo ndogo kuanzia shilingi 50, 100, 200 na 500 na kusababisha mfumuko wa bei kwenye masoko yetu madogo madogo.

Je, Wizara inalitambua hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninamuomba tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hili tulichukue tukalifanyie kazi, tukafuatilie tuone kwamba hivyo ndivyo hali halisi ilivyo na tuone ni njia gani ya kulipatia utatuzi suala hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Serikali sasa ina mpango gani wa kuendeleza mkopo wa wanawake maarufu kama Mama Samia, ambao ulitangazwa kwenye Manispaa zetu na wanawake wakajitokeza kuomba mikopo hiyo, Serikali ina mpango gani wa kuuendeleza mkopo huo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo litaenda Serikalini kama swali la msingi kwa sababu swali lililoko hapa Waheshimiwa linahusu fedha za *PRIDE*. Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusimamia taasisi ndogondogo zinazoumiza wananchi katika mikopo yake kama hizi zinazojulikana kama kausha damu, komandoo, rusha roho na kadhalika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango na mikakati na ndiyo maana tumeanzisha sheria na taratibu kwa hiyo taasisi yoyote ambayo inaanzisha mikopo lazima ifuate sheria na taratibu na iwe imesajiliwa na Benki Kuu ya Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali italipa madai ya waliokuwa wakulima wa mashamba makubwa ya maua na mboga mboga ya *Killiflora* katika Mkoa wa Arusha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo nalo liende kama swali la msingi. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Yaliyotokea Mtwara Mjini kwa *PRIDE* pia yametokea ndani ya Iringa Manispaa. Je, zoezi hilo Julai mtalifanya kwa wote nchi nzima pamoja na Iringa Manispaa walioathirika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jesca kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tuliposema kwamba Kampuni hii ya *PRIDE* tayari imefanyiwa taratibu na Sheria ya Ufilisi, tunaenda kulipa fedha hiyo kwa wadai walioko Mtwara nina maana kwamba ni nchi nzima wale ambao wana madai Julai tutaanza kulipa fedha hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile Mbunge wa Kigamboni swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji.

Na. 576

**Serikali kuruhusu mifumo ya malipo ya kimataifa**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza:-

Je, lini Mifumo ya Malipo ya Kimataifa itaruhusiwa ili wabunifu/watu wanaofanya kazi za ushauri kwa taasisi za nje wapate malipo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa ya mwaka 2015 inawataka watoa huduma za mifumo ya malipo kupata leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania ili kutoa huduma hizo nchini. Utaratibu huu unaiwezesha Benki Kuu kuwa na usimamizi wa moja kwa moja kwa watoa huduma za mifumo ya malipo nchini na

kuhakikisha panakuwa na mifumo ya malipo inayoaminika na salama kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sheria hiyo, Benki Kuu imeweza kutoa leseni kwa watoa huduma za mifumo ya malipo wa kimataifa ambapo wamefungua ofisi zao nchini, ambapo hadi Aprili mwaka 2023 jumla ya taasisi 10 za kimataifa ambazo si benki za biashara zimepewa leseni ya kutoa huduma za mifumo ya malipo nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa leseni za kutoa huduma za mifumo ya malipo zinatolewa kwa watoa huduma wote, wa ndani na nje ya nchi, waliotayari na wanaokidhi matakwa ya sheria ili kutoa fursa kwa wananchi kupata huduma stahiki za mifumo ya malipo zinazozingatia usalama wa fedha zao na maslahi mapana ya nchi. Ahsante

.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji swali la nyongeza.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya ziada. Namshukuru Waziri kwa jawabu lake zuri lakini ningeomba sasa Serikali ituambie, kwa sababu vijana wanapata tabu sana kupata malipo yao, Je, ni lini Serikali itaruhusu mifumo kama ya *PayPal* ili watu waanze kulipwa fedha zao? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zahor kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *PayPal* haijaomba leseni. Mara tu itakapoomba leseni na kukidhi vigezo vya kisheria basi Serikali itaruhusu kampuni hiyo kutoa huduma nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ilikuwa niseme kwa niaba yake kwa sababu aliwasiliana na mimi pia. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri malizia pale alipoishia Naibu Waziri wa Maji majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, samahani naomba kidogo tu unikumbushe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kasema pesa zimekwama kwenu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba hili tulichukue tukalifanyie kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 577

**Ujenzi wa barabara ya Arusha – Simanjiro – Kongwa**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Arusha – Mirongoine – Simanjiro – Terati hadi Kongwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Arusha – Mirongoine – Simanjiro – Kongwa inajulikana kwa jina la Arusha – Kibaya – Kongwa yenye urefu wa kilometa 453. Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa *Engineering, Procurement, Construction plus Finance (EPC + F)*. Hadi sasa Mkandarasi amekwishapatikana na mkataba wa ujenzi utasainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2023. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, barabara hii inahudumia mikoa mitatu Arusha, Manyara na Dodoma. Je, Serikali haioni sasa ni muhimu kuharakisha barabara hii ili kujenga uchumi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, kwa kuwa barabara hii iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020/2025, Serikali haioni kutoharakisha barabara hii ni kutotekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020/2025? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili kwa pamoja ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi, ni kweli barabara hii iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini pia ni kweli inaunganisha Mikoa mitatu, kwa maana hiyo ndiyo maana katika jibu langu la msingi hii barabara imetengewa fedha na tumeipitisha inaanza kujengwa kwa *EPC+F* na kama nilivyosema tutaisaini kuanza ujenzi wa barabara hii kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha kwa mwaka huu, kwa maana ya huu mwezi Juni. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ningependa kujua ni lini barabara ya kiusalama kutoka Susuni – Mwema - Sirari – Mriba – Nyamongo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami mara tu tutakapokuwa tumekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Athuman Bushiri swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Makanya – Ruvu ambayo inakwenda kwenye machimbo ya *gypsum? (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ni barabara ya kimkakati ambayo inaenda kwenye maeneo muhimu ya kiuchumi. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Norah Mzeru swali la nyongeza.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii; je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati barabara ya kutoka Nanenane – Tungi kupita *VETA* kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba arudie alipotaja vituo viwili vya mwisho sikumsikia vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Norah Mzeru.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati barabara ya kutoka Nanenane – Tungi kupitia *VETA* kwa kiwango cha lami Mkoa wa Morogoro? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na utaratibu wa kufanya matengenezo ya barabara zote kwa kiwango cha lami, kwa hiyo hata mwaka unaokuja wa fedha tumetenga kwa ajili ya kukarabati maeneo yote ambayo yameharibika ili kuhakikisha kwamba barabara inarudi kwenye ubora wake. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kuna changamoto kubwa sana ya mlundikano wa malori ndani ya Mji wa Tunduma ambao unasinyaza na kufubaza uchumi wa Wana-Tunduma. Serikali mna mpango gani wa kujenga njia ya dharura ili kunusuru hali iliyopo kwenye Mji wa Tunduma? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna msongamano mkubwa sana katika Mji wa Tunduma ambao ndipo tunapotoka pale kwenda Zambia. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Tunduma kwamba tunakwenda siyo tu kufanya mpango wa dharura, lakini mpango kamili wa kujenga barabara ya njia nne katika Mji wa Tunduma ambapo tutakwenda kujenga kwa mpango wa *EPC+F*.

Mheshimiwa Spika, moja ya maeneo ambayo tunategemea kuanza ni pamoja na miji ya Tunduma ili kukwamua na kuondoa changamoto ambayo ipo inayosababisha msongamano mkubwa katika Mji wa Tunduma. Kwa hiyo, mkataba huo tunategemea utasainiwa Juni mwaka huu wa fedha, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hiyo. Barabara ya Kolandoto kwenda Kishapu ina kero kubwa kwa wasafiri na wasafirishaji. Ni lini Serikali itaanza kutekeleza mradi huu katika kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya Kolandoto - Kishapu – Lalago, ni moja ya barabara kuu na Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba katika mpango huu wa fedha kwa maana ya bajeti ambayo tumepitishiwa, tayari tumeshatenga fedha kwa ajili ya kuanza kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Barabara ya Kigamboni mpaka Kongowe eneo la Mikwambe lina tatizo ya mifereji: Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mifereji katika barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja, siyo tu mifereji, bali pia ni barabara ambayo kuna vipande vingi ambavyo vimechoka sana. Kwa hiyo, mpango wa Serikali pamoja na kutengeneza mifereji, pia ni kukarabati yale maeneo yote ambayo yamechakaa sana, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itaridhia ombi la Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro la kupandisha hadhi kuwa barabara za Pofo - Mandaka - Kilema, barabara ya Uchira – Kisomachi - Kolarie na ile ya Kahe *TPC*?

**SPIKA:** Mheshimiwa, hiyo ni barabara moja au ni barabara tatu tofauti?

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ni tatu.

**SPIKA:** Unataja moja kwa sababu ni swali la nyongeza. Chagua moja kati ya hiyo ili Mheshimiwa ajibu.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ni lini mtapandisha hadhi barabara ya Uchira – Kisomachi - Kolarie?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge, kuhusu kupandisha hadhi hizi Barabara, kuna taratibu zake, ambapo kama Mheshimiwa Mbunge pamoja na vikao vya kuanzia wilaya, mkoa wataleta maombi, Wizara ya Ujenzi ambayo watakwenda kufanya tathmini na baada ya hapo kama itakidhi vigezo, maana yake ni kwamba hiyo barabara itakuwa imepandishwa hadhi. Pia kama itakuwa barabara hiyo haikupandishwa hadhi, wanaweza kuomba kukasimiwa kukarabatiwa ama kusimamiwa na *TANROADS,* ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Je, Serikali haioni kwamba ni busara kukamilisha barabara ya Kilosa kwenda Mikumi ili kuongeza tija kwenye uwekezaji mkubwa wa reli ya *SGR* pale Kilosa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, nimesikia tu barabara ya Kilosa – Mikumi, lakini swali sikumsikia anataka nini hasa Serikali ifanye.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nimeuliza hivi: Je, Serikali haioni kwamba ni busara kukamilisha kipande cha barabara kutoka Kilosa kwenda Mikumi ili kuipa hadhi na kuongezea thamani reli yetu ya *SGR* pale Kilosa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge wa Mikumi, siyo tu busara, lakini kwa kweli ni barabara ambayo ni muhimu, ambayo sasa itakuwa inaunganisha barabara ambayo tunaijenga kwa *EPC* kuanzia Namtumbo – Malinyi – Mikumi ambayo tunaona busara badala mtu kwenda Morogoro, itoke Mikumi kuja Kilosa. Kwa hiyo, hiyo mipango ipo kuhakikisha kwamba tunapafungua kati ya Kilosa na kuunganisha na Mikumi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara inayoanzia Nanganga kwenda Ruangwa inajengwa sasa kwa kiwango cha lami. Hata hivyo…

**SPIKA:** Swali, swali, swali.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, wakazi wa Nanganga wanadai fidia. Ni lini Serikali italipa fidia kwa watu waliobomolewa nyumba zao eneo la Nanganga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:_

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na utaratibu wa kulipa fidia tunapoanza ujenzi wa barabara zote. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, kama kuna changamoto kwa hiyo barabara, tuweze kuonana ili tujue tatizo ni nini ambapo wananchi hao wanaodai mpaka sasa hivi wakati barabara inajengwa na tulitatue kwa kuwalipa fidia hao wananchi wa barabara ya Nanganga hadi Ruangwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma swali la nyongeza.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, Serikali imefikia hatua gani katika maandalizi ya kuijenga barabara ya Haydom -Mogitu kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara ya Mogitu - Haydom ni barabara ambayo ni *link* kwenye ile barabara ya Karatu - Mbulu – Haydom kwenda Lalago. Kwa hiyo, ni *link* ya hiyo barabara. Kwa hiyo, ni sehemu ya hiyo barabara, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga kilometa kumi za lami kwenye mitaa ya Mji wa Bunda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI, ipo mipango ya kutimiza hiyo ahadi ya kujenga barabara ya kilometa kumi ambazo ziliahidiwa na viongozi wetu katika Mji wa Bunda kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mbuguni kwa kiwango cha lami ambayo inaanzia Tengeru hadi Mererani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, ni ya kimkakati ambayo inakwenda machimbo ya Tanzanite. Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi kwamba mpaka sasa hivi tunaendelea kukamilisha usanifu wa kina na baada ya hapo Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga sasa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, swali la nyongeza.

**MHE. ASKF. JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kwamba barabara ya kutoka Bunju B mpaka Mabwepande ijengwe kwa kiwango cha lami katika Jimbo la Kawe: Ni lini Serikali itatimiza ahadi hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya Bunju B – Mabwepande – Magohe – Mapigi hadi Kibamba, ni moja ya barabara ambayo sasa hivi inafanyiwa usanifu. Siyo tu ahadi ya viongozi, lakini tunategemea ndiyo itakuwa *altering* ya barabara za Mji wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, ipo kwenye mpango na

tunavyoongea sasa hivi Washauri Wahandisi wako kazini wanafanya usanifu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

Na. 578

**Ujenzi wa barabara ya Bungu – Nyamisati, Kibiti**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Bungu hadi Nyamisati Wilaya Kibiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* inaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Bungu hadi Nyamisati yenye urefu wa kilometa 40.03. Kazi ya usanifu inatarajiwa kukamilika tarehe 30 Juni, 2023. Baada ya kukamilika kwa usanifu, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali: Je, mko yatari kuanza sasa usanifu na ujenzi wa barabara hiyo kwenye bajeti ya mwaka huu unaokuja Julai, 2023/2024?

**SPIKA:** Mheshimiwa, mtajie mwaka vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, mko yatari kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwenye bajeti inayokuja 2023/2024?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi, nilisema tunakamilisha usanifu wa kina mwezi huu tarehe 30 Juni. Tayari bajeti imeshapitishwa. Kwa hiyo, hiyo barabara itaingizwa kwenye mpango wa mwaka unaofuata kwa ajili ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyonyeza. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kuanzia Gairo – Chanjale - Kibakwe hadi Mpwapwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hiyo ni barabara moja?

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, hiyo ni barabara moja.

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ishengoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii barabara ilifanyiwa usanifu wa awali na bado haijafanyiwa usanifu wa kina. Kwa hiyo, barabara hii ikishafanyiwa usanifu wa kina, Serikali itakuwa imefahamu gharama ya hiyo barabara na ndiyo tutaanza sasa kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Barabara ya Bungu - Nyamisaki ni barabara ya muda mrefu sana kabla hata bandari haijajengwa. Tumeuliza haya maswali humu muda mrefu na siku nyingi na kila tukiuliza wanasema tutajenga. Tunaomba *commitment* ya Serikali, barabara hii mtaijenga lini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Kikwete Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii ni ya siku nyingi na tunatambua umuhimu wake kwamba barabara hii ndiyo inayounganisha Pwani na Kisiwa cha Mafia. *Commitment* ya Serikali kama nilivyosema, ndiyo maana sasa tumeamua kuifanyia usanifu yakiwa ni maandalizi kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, tunavyoongea, kazi inaendelea. Kwa hiyo, tuna hakika baada ya kukamilisha usanifu, barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Barabara ya kutoka Ifakara – Lumemo – Michenga – Idete mpaka Mlimba imeshatangazwa; je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante ni kweli kwamba barabara hiyo imeshatangazwa na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajenga kilometa 100 na tuna *lots* mbili. Kinachosubiriwa sasa hivi ni kusaini mikataba na wakandarasi ambao wamepatikana kwa ajili ya kuanza ujenzi huo wa barabara, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Barabara ya Nyoni - Maguu inayopitia Mawono kwenye mlima mkali, ni lini tutaanza ujenzi kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara anayoitaja Mheshimiwa Kapinga ni kweli, na ipo kwenye ilani kwamba ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kuijenga, lakini kitu ambacho tunategemea tukifanye kwanza ni kuhakikisha kwamba yale maeneo yote yenye miinuko tunajenga aidha kwa zege ama kwa lami nyepesi ili kupunguza changamoto kwa wasafiri ambao wanasafiri katika hiyo barabara ya Nyoni – Maguu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 579

**Ujenzi wa barabara ya Kilwa kwa Njia Nne**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa njia nne kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Kilwa kipande cha Mbagala Rangi Tatu hadi Kongowe utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa kipande cha barabara kutoka Mbagala Rangi Tatu hadi Kongowe, kilometa 3.8 katika mwaka wa fedha 2023/2024, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali langu la kwanza la nyongeza, napenda kujua, ni lini Serikali itakarabati kipande cha barabara toka Somanga hadi Nangurukuru hadi Mbwemkuru ambacho kimechakaa sana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; miaka ya hivi karibuni Serikali ilitanua barabara za mikoa na barabara kuu katika Mkoa wa Lindi, lakini haijaweza kulipa fidia hadi wakati huu. Ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi walio kando kando ya barabara hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii kuu ya Kusini Somanga - Nangurukuru hadi Mbwenkulu hadi Mnazi Mmoja imechoka. Hii barabara sasa hivi inapitisha mizigo mizito sana tofauti na ilivyokuwa awali. Kwa hatua za haraka ni kukarabati yale maeneo yote ambayo yamechakaa sana ili kuhakikisha kwamba hatukwamishi magari. Mpango mkubwa wa sasa hivi, Serikali inatafuta fedha ili kuifanyia ukarabati wa barabara yote kuendana sasa na uzito wa magari ambayo yanapita kwenye hiyo barabara ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kwamba tulibadilisha sheria kwa maana ya kuongeza upana wa barabara. Wizara ya Ujenzi inachofanya sasa hivi ni kufanya tathmini kwa barabara zote. Kwa kuanzia, pale ambapo tunaanza ujenzi, tunalipa, lakini tunataka tupate gharama nzima kwa barabara zote ambazo zimeongezeka kwa ajili ya kutafuta fedha kuwafidia wananchi ambao barabara imewafuata, na siyo kwa Lindi tu, ni kwa sehemu kubwa ya nchi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kipande hicho cha Mbagala Rangi Tatu hadi Kongowe kinakuwa na msongamano mkubwa wa magari kiasi kwamba ni foleni masaa yote: Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi kuhakikisha wanapanua ile barabara ili magari yaweze kupita na kuepukana na foleni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tunatambua changamoto ambayo ipo kwenye hii barabara na ndiyo maana tumeiweka kwenye mpango. Serikali itakachofanya ni kuhakikisha kwamba inaanza haraka ujenzi wa kipande hiki ili kuondoa adha ambayo inawakuta wananchi ambao wanatumia hii barabara ikiwa ni pamoja na kupunguza msongamano kwa maana ya kupunguza muda mwingi ambao unatumika katika kipande hiki. Ndiyo maana tayari tumeshaingiza kwenye mpango. Kwa hiyo, cha msingi ni kuanza haraka ujenzi wa barabara hii kwa hizo njia nne, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa barabara ya kuingia Singida Mjini, almaarufu kama barabara ya Kibaoni, imekuwa finyu: Ni lini Serikali itaitanua barabara hiyo na kuwa njia nne?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kinachofanyika ni *study* ya miji yote ambayo inaendelea kukua na Singida ikiwa mojawapo. Kwa hiyo, tunaendelea kufanya *study* kwenye miji mbalimbali ambayo tunaona kunahitajika kupanuliwa kwa barabara hasa zinazoingia kwenye miji. Hii ni pamoja na miji kama hii ya Dodoma, Singida ambayo tunaona kadiri kunapokucha magari yanaongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea na usanifu wa hizo barabara ili tuone kama zinahitajika njia nne, ama njia sita, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuna wananchi wengi wa Mwibara uliopisha mradi wa barabara kati ya Bulamba na Kisorya imechukua muda mrefu kweli bila kulipwa. Sasa

naomba *commitment* ya Serikali: Ni lini wananchi hawa watalipwa fidia zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu wakati najibu muuliza swali la msingi wananchi ambao bado hawafidiwa ni wale ambao wako kilomita I *mean* wako mita 7.5 kutoka kwenye barabara na ndiyo maana nilisema tunafanya tathimini ya nchi nzima. Wamepewa kazi hiyo wale Mameneja wa Mikoa kuangalia na kufanya tathimini ili tupate gharama halisi ili wakati Serikali inalipa basi iweze kujua gharama halisi ya fidia ambayo inatakiwa kulipwa ikiwa ni pamoja na wananchi wa Mwibara ambao wamepisha barabara hiyo ya Kisorya ya Bulamba, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nitaleta matangazo niliyonayo hapa mbele lakini pia nitakuwa na taarifa ya kuwapa.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na tangazo la wageni. Tunaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika, ninaowageni leo ambao ni wanamaombi kutoka Mikoa mbalimbali wakiongozwa na Mchungaji Mary Msigwa, karibuni sana. Mchungaji Mary Msigwa ameongozana na Ndugu Judith Chamwela, Ndugu Imirda Mavukilo, Ndugu Theophili Kichiba, Ndugu Stivini January, Ndugu Sara Zuberi, Ndugu Devota Mlohe na Ndugu Agnesi Msigwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni wengine ambao wanatoka *Dodoma Sports Company Limited*. Hawa ni waandaji wa Mashindano ya Mbio za Barabarani za *Capital City Marathon* zitakazofanyika tarehe 11 Juni, 2023. Hawa timu nzima iko hapo lakini

wanaongozwa na Ndugu Nsolo Mlozi ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa *Capital City Marathon* na Ndugu William Kalaghe ambaye ni Makamu wa Rais wa Shirikisho la Riadha Tanzania, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Ndugu Alhaj Said Sultan Sidde ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ilala, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Shaaban Mussa, Diwani Kata ya *Pugu Station*, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Murtaza Darugar ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Kata ya Kisutu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Zeenat Walimohamed, Katibu wa CCM Kata ya Kisutu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Mohamedali Versi ambaye Mwenyekiti wa Wazazi Kata ya Kisutu, karibu sana. *(Makofi)*

Lakini pia yupo Ndugu Abidi Hussein ambaye hapa tangazo nadhani kuna maneno wamesahau lakini naona ni Kiongozi wa Vijana hapa wameandika Mjumbe wa Halmashauri ya CCM Vijana, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni wageni 35.

Waheshimiwa Wabunge, mnaozungumza na mnaoongea na simu sitachoka kuwakumbusha, tawakumbusha kila siku mpaka siku nitakayoanza kutaja jina moja moja ndiyo watu mtaacha. Lakini kwa sasa sitachoka kuwakumbusha taanza kutaja jina moja moja kila mtu atakuwa anakumbuka hataki kutajwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Viongozi wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa

Chama cha Mapinduzi Jimbo la Ilala Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Juma Mizungu ambaye ni Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Ilala, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali wa kwetu sisi sote humu ndani; tunao wageni watano wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambao wanatoka Jimbo la Sikonge, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Haji Makame Mlenge ambao wanatoka Jimbo la Chwaka, Kusini Unguja, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Kavejuru Felix ambao ni kutoka Buhigwe Mkoa wa Kigoma, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 42 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ambao ni Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji, Walimu kutoka Kintinku Mkoa wa Singida, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 39 wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni walimu na wafanyakazi waliyofanya vizuri kutoka Kata ya Yaeda Chini wakiongozwa na Diwani Mheshimiwa Braisoni Magombe, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambaye ni Mbunge wa Kigamboni na hawa ni *Runners Club* kutoka Kigamboni, Mkoa wa Dar es salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 24 wa Mheshimiwa Silyvestry Koka ambao ni Kamati ya Siasa ya Wilaya na Wajumbe wa Mfuko wa Jimbo kutoka Kibaha Mjini Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 17 wa Mheshimiwa Zuena Bushiri ambao ni kikundi cha wamama wajasiriamali kutoka

Moshi Mjini Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Rehema Migilla mbaye anatoka Ulyankulu Mkoa wa Tabora, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Zaytun Swai ambao ni wanafunzi wenzake waliyosoma naye *Master's* katika Chuo cha Strathclyde Scotland, karibuni sana, karibuni sana. Hapa wameandikwa tisa sijui pengine wengine hawajapata nafasi haya. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Robert Maboto ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Bunda, haya nafikiri hawa ni wageni ambao wamekosa nafasi hapa ndani leo ama, ahaa naambiwa wamekaa hii sehemu ya watalamu haya karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ambao ni Wachungaji kutoka Tarime, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Samweli Hhayuma ambao ni Viongozi wa Kata ya Garawaja wa Chama cha Mapinduzi kutoka Hanang, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Hamisi Taletale kutoka Jijini Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi kutoka Malinyi Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Kwanza mtagundua kwa nini nahitaji kuanza kutaja majina yaani hapa hapa na nimesimama na tangazo limetoka hapa hapa na Mawaziri wanazungumza. Kwa hiyo, mpate mtihani ulivyo.

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo tunao wanafunzi 53 na wazazi wanne kutoka shule ya Sekondari *Precious Blood* ya Jijini Arusha, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 120 na walimu 12 kutoka Shule ya Sekondari Ikoa ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu kutoka *TBC,* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tuliyonao siku ya leo ama asubuhi hii Bungeni na nimejulishwa hapa kwamba tulikuwa na wageni wengi zaidi lakini hawajapata nafasi ya kuingia hapa ndani kwa sababu ya nafasi. Kwa hiyo, sijui kama watapata nafasi ya kuingia ama tutaangalia utaratibu mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, ratiba yetu ya leo tuliyokuwa tumewagawia ilikuwa inaonyesha kwamba leo kungewasilisha Taarifa ya Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu changamoto za utekelezaji wa Mkataba wa Mauziano ya Matrekta ya Kampuni ya *URSUS* kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* na Wakulima.

Waheshimiwa Wabunge kama inavyoonekana katika ratiba Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge unaoendelea leo. Leo Ijumaa 09 Juni, 2023 tulitarajia kupokea Taarifa ya Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu changamoto za utekelezaji wa Mkataba wa Mauziano ya Matrekta ya Kampuni ya *URSUS* kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* na Wakulima kwa utaratibu wa mkopo.

Waheshimiwa Wabunge katika kutekeleza jukumu lake kuhusu kuchunguza ukweli wa changamoto na malalamiko yaliyojitokeza kwenye utekelezaji wa Mkataba huu Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ilifanya Ziara katika Wilaya za Kiteto, Hanang na Babati Mkoani Manyara ambayo kwa kiasi kikubwa iliathirika na Mkataba huo.

Waheshimiwa Wabunge hata hivyo mpaka wakati wa kukamilisha uchambuzi wa taarifa yake Kamati haikuweza kupokea ripoti kadhaa ambazo ni muhimu katika kukamilisha taarifa yake ya uchunguzi. Ripoti hizo ni pamoja na hizi zifuatazo: -

(i) Taarifa ya Kamati iliyoundwa na Katibu Mkuu kwa ajili ya kuchunguza ubovu wa matrekta;

(ii) Taarifa ya *NDC* kuhusu namna ilivyozingatia ushauri wa *CAMARTEC* baada ya ukaguzi wa matrekta;

(iii) Barua na Taarifa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali akitoa ushauri wa kisheria baada ya upekuzi wa mikataba;

(iv) Taarifa ya Kampuni ya udalali ya majembe ya namna walivyoendesha zoezi la kukusanya marejesho kutoka kwa wakulima;

(v) Taarifa ya TAKUKURU kuhusu oparesheni ya marejesho ya mikopo ya wakulima;

(vi) Taarifa ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu mtiririko wa fedha zote *(cash flows)* zinazohusiana na mradi wa matrekta ya *URSUS* na;

(vii) Taarifa ya upekuzi *(due diligence)* kwa Kampuni ya *URSUS*.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa kukosekana kwa taarifa hizo nilizozitaja hapo juu kumesababisha kutokujitosheleza kwa uchambuzi wa Kamati. Nimeona ni vema Taarifa ya Kamati kuhusu jambo hili isiingie Bungeni leo kama jinsi ilivyokuwa imepangwa kwenye ratiba ya Mkutano huu hadi hapo Kamati itakapokamilisha kazi yake kwa kupata nyaraka zote muhimu inazozihitaji. Aidha, nitumie fursa hii kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya mpaka ngazi hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo la katibu linalotoka kwa Katibu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itaendesha Semina kuhusu mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu na Mafunzo. Semina hii itafanyika siku ya Jumapili tarehe 11 Juni, 2023 saa nne asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnakaribishwa kuhudhuria Semina hii muhimu ili kuwajengea uelewa kuhusu Mapendekezo ya Maboresho ya Sera na Mitaala ya Elimu pamoja na kupata maoni na ushauri wenu. Kwa hiyo, mnasisitizwa Waheshimiwa Wabunge kuhudhuria. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa siku ya kesho tunakusudia kukutana kwa mujibu wa ile ratiba yetu tuliyowagawia. Sasa Kanuni zetu mnafahamu zinaweka muda wa kukutana, kwa hivyo nimwite Mheshimiwa Waziri ili aweze kuleta kwenu hoja ya kutengua Kanuni. Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nitoe maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 174(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge umepangwa kufanyika kwa siku 59 za kazi. Kuanzia tarehe 04 Aprili, 2023 hadi tarehe 30 Juni, 2023 na kwa kuwa tarehe 23 Mei, 2023 Kamati ya Uongozi ilikaa ili kuzingatia shughuli za nyongeza zilizoletwa na Serikali na iliazimia kwamba Siku ya Jumamosi tarehe 10 Juni, 2023 Bunge likae ili kujadili Shughuli zilizoongezeka.

Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa Kanuni ya 34(15) inaelekeza kwamba Bunge halitaendelea na shughuli zake siku ya Jumamosi, Jumapili au Siku ya Mapumziko na kwa kuwa shughuli zilizopo haziwezi kufanyika kwa ufanisi na kukamilika ndani ya muda wa siku 59 zilizotengwa kwa ajili ya Mkutano huu hivyo basi ili kuliwezesha Bunge kutekeleza kazi zake kiufanisi na kuweza kumaliza shughuli

zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano wa Kumi na Moja. Kanuni ya 34(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari Mwaka 2023 itenguliwe ili Bunge likutane siku ya Jumamosi 10 Juni, 2023 isipokuwa kwamba siku hiyo Bunge litaanza Saa Tatu Asubuhi hadi Saa Nane Mchana na hakutakuwa na kipindi cha maswali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Ilitolewa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kutengua Kanuni iliafikiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nyie mliokaa hamtaki tukutane kesho kwa ajili ya kujadili? Haya nawaona ambao mmekaa kesho msilete vikaratasi kwa kuomba kuchangia hapa mbele. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kwa mujibu wa taratibu zetu. Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya kutengua Kanuni ili Bunge liweze kukutana kesho hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu waseme ndiyo, wasioafiki waseme siyo. Wasioafiki ni wawili tu, kwa hiyo walioafiki wameshinda, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo niliokuwa nimeyatoa hapo awali kwa sababu Kamati ambayo ilikuwa ilete taarifa leo haitaweza kufanya hivyo. Kwa sababu haijakamilika basi naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 04.37 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi,*
*Tarehe 10 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*